MWONGOZO (MANUAL)

JINSI YA KUTHIBITISHA NA KUGHAIRI UDAHILI (HOW TO CONFIRM AND UNCOFIRM)

Hatua #1: Tembelea tovuti yetu www.juco.ac.tz

Kama umeandika tovuti kwa usahihi, itakupeleka kwenye tovuti yetu kama inavyoonekana kwenye Hatua #2.

Hatua #2: Bofya **"Apply Now"** au **"Click here to apply now"**



Hatua #3: Bofya tena "**Apply Now**"



Ukibofya kwa usahihi, mfumo utakupeleka moja kwa moja sehemu ya Login.

Hatua #4: Nenda sehemu ya "**Login**"



Utaona sehemu inayokuhitaji kujaza taarifa kama inavyoonekana hapa chini. Sehemu ya Username*, jaza namba yako ya mtihani kidato cha 4 (*Form IV Index number*); weka nywila (*password*) kisha bonyeza* **Login** *(kama inavyoonekana hapa chini)*



Hatua #5: Kupata Nywila Mpya (To Get a New Password)



Bofya Forgot your password? *Kisha, bofya* **Login.** *Mfumo utakupeleka kwenye sehemu ya kujaza* **username** *yako, jaza kwa usahihi, kisha* bonyeza "**Reset Password**"

Mfano:



Ikiwa umejaza **Username** *kwa usahihi, utapokea* nywila (password) mpya *kwa njia ya SMS katika simu yako.*

Angalia ujumbe (SMS) kisha endelea kuanzia *Hatua #4.*

Mfano wa SMS ya nywila (password) mpya utakayopokea:



Hatua #6: Kuthibitisha Udahili (To Confirm Admission)

Ikiwa umechaguliwa chuo zaidi ya kimoja, akaunti yako itakuwa na ujumbe unaosomeka ifuatavyo:



Ingiza confirmation code ulizotumiwa na TCU kisha bonyeza Confirm. Utaona ujumbe kama unaoonekana katika mfano hapo chini.



Ikiwa haujatumiwa **Confirmation Code** kutoka TCU,



Bonyeza ***Request Confirmation Code*** *Kisha, jaza namba ya simu ambayo ungependa ipokee code husika. Hakikisha namba inaanza na 255. Jaza baruapepe (e-mail) yako, kisha bonyeza*



Ikiwa umejaza namba na baruapepe (e-mail) kwa usahihi, utapokea ujumbe mfupi (SMS) kama inavyoonekana hapa chini:



Ukishapokea **Confirmation Code**, *rudi kwenye akaunti yako ya JUCo-OAS kama inavyoonekana kwenye* ***Hatua #6.***

Hatua #7: Kupata Barua ya Udahili (To Get Admission Letter)

- *Ingia katika akaunti yako kisha bonyeza sehemu iliyoandikwa* Get Admission Letter



- *Ukishabonyeza, barua hiyo itafunguka kwa mfumo wa* **PDF**.

Hatua #8: Kughairi Uthibitisho wa Udahili (To Unconfirm Admission)

(a) Angalia upande wa juu-kulia panapoonesha jina lako. Bonyeza alama ya pembetatu inayoonekana mbele ya jina lako. Zingatia alama nyekundu hapo juu.

(b) Kisha bonyeza Unconfirm au kipengele kingine kwa kadri ya lengo lako.



KWA MAULIZO (FOR ENQUIRIES):

0717 781 455 | 0783 659 567 | 0756351329 | 0765 660 606